# Mastaajabu ya Nguvu za Kubariki

Richard Brunton

# Mastaajabu ya Nguvu za Kubariki

Richard Brunton

Mastaajabu ya Nguvu za Kubariki
Kimetangazwa na Richard Brunton Ministries
Nyuzilandi

Hakimiliki © 2017 Richard Brunton

Second edition

ISBN 978-0-473-42987-4 (Softcover)
ISBN 978-0-473-42988-1 (ePUB)
ISBN 978-0-473-43025-2 (PDF)

Uhariri:
Shukrani maalum kwa
Joanne Wiklund na Andrew Killick
Kwa kuifanya hadithi isomeke zaidi ya vile
pengine vinginevyo ingewezekana!

Utoaji na upigaji chapa:
Andrew Killick
Castle Publishing Services
www.castlepublishing.co.nz

Mchoro wa jalada:
Paul Smith

Manukuu ya maandishi matakatifu yametolewa katika
New King James Version
Hakimiliki © 1982 na Thomas Nelson Inc.
Yametumika kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa.

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA
Hakuna sehemu yoyote ya chapa hii inayoweza kutolewa tena,
kuhifadhiwa katika mitambo inayoweza kutoa upya, au kutumwa kwa
namna yoyote au kwa njia yoyote, ya kieletroniki, kimashine, kufotokopi,
kurekodi bila idhini ya mchapishaji.

# YALIYOMO


Dibaji 5
Utangulizi 9

**Sehemu ya Kwanza: Kwa Nini Kubariki? 13**
Utambuzi 15
Uwezo wa Unenaji Wetu 19
Kutoka Katika Unenaji Mzuri Hadi Kubariki… 22
Baraka ya Kikristo Ni Nini? 24
Mamlaka Yetu ya Kiroho 27

**Sehemu ya Pili: Namna ya Kukifanya 33**
Baadhi Ya Kanuni Muhimu 35
    Fanya kinywa chako kunena mema 35
    Uliza Roho Mtakatifu utakachosema 35
    Baraka ilivyo tofauti na uombezi 36
    Usihukumu 37
    Mfano wa kuelezea 38
Hali Tofauti Tofauti Tunazo Weza Kukabili 40
    Kubariki wale ambao hukushutumu… 40

Kubariki waliokujeruhi au kukukataa 41
Kubariki wale ambao wamekuchokeza 44
Kujibariki Badala ya Kujilaani 47
Kutambua na kuvunja laana 47
Kujibariki mdomo 49
Kujibariki fikira 51
Kujibariki miili yetu 52
Kubariki nyumbani, ndoa na watoto wako 57
Baraka ya baba 65
Kubariki wengine kwa kuachilia kinabii 69
Kubariki mahali pako pa kazi 70
Kubariki jumuia 73
Kubariki ardhi 74
Kubariki Bwana 76
Neno la mwisho kutoka kwa msomaji 77

Kutumia 78
Namna ya Kuwa Mkristo 80

# DIBAJI

Ninakuhimiza ukisome hiki kitabu kidogo chenye ujumbe wa nguvu – utabadilishwa!

Ilikuwa Richard Brunton na mimi tulipokuwa tunatumia kiamshakinywa asubuhi moja kwamba alinishirikisha katika kile Mungu alikuwa amemfunulia kuhusu nguvu za kubariki na mara niliona uwezekano wa matokeo makubwa katika maisha ya wengine.

Nilikumbatia ujumbe wake kuonyesha katika mkutano wa wanaume wa kanisa letu. Wanaume waliokuwepo walifikiri ulikuwa mzuri sana hadi wakataka kanisa lote liusikie. Watu walianza kuufanya mazoea katika kila sehemu ya maisha yao na tulisikia shuhuda za kustaajabisha kama matokeo. Mfanyabiashara mmoja alisimulia kwamba biashara yake ilikuwa imetoka si kitu hadi faida katika wiki mbili. Wengine waliponyeshwa kimaumbile kama walivyojibariki miili yao.

Fursa zingine kwa ajili ya ujumbe huu kusikika zilianza kujitokeza. Nilikuwa nakaribibia kuhututubu katika kongamano la Majemedari (ambapo Mapasta wa makanisa huja pamoja kujifunza na kufanywa wapya) katika Kenya na Uganda. Richard aliambatana nami katika kubariki. Ujumbe ulipenyea katika utupu na uchungu uliodumu muda mrefu. Wengi wa watu waliohudhuria hawakuwahi kubarikiwa na baba zao na Richard aliposimama katika nafasi ile na kuwabariki, wengi wao walilia na kuhisi mshtuko na ukombozi wa kiroho pamoja na mabadiliko katika maisha yao mara hiyo.

Kujua namna ya kubariki kumebadilisha maisha yangu hadi kiwango cha mimi kutafuta fursa za kuwabariki wengine katika 'neno na tendo'-kupitia nisemacho na nifanyacho. Utakifurahia kitabu hiki kidogo na ukikitumia katika maisha yako, matokeo yako mema yatajaa tele na kufurika kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

**Geoff Wiklund**
Geoff Wiklund Ministries,
Chairman, Promise Keepers,
Auckland, Nyuzilandi

Mungu amembariki Richard na ufunuo wa nguvu za baraka zinapoachiliwa kwa wengine. Ninaamini kwamba, huu ni ufunuo wa sasa kutoka kwa Mungu. Richard anapoishi katika ufunuo na ujumbe wake, haya yanaleta uhalisia ambao watu wanaweza kuihusisha nao mara moja.

Hii ilisababisha tumwalike Richard kuzungumza katika mikutano yetu yote ya shughuli za wanaume wa Promise Keepers. Matokeo ya ujmbe huu yalikuwa yenye nguvu na ya kubadilisha maisha ya wengi.

Ujumbe wa 'Baraka' uliwafikia wengi na kuchukua kwa nguvu nyoyo za wanaume wengi katika mikutano za Promise Keepers. Watu wengi walikumbatia ujumbe huu muhimu wa baraka, kuomba na nguvu za kunena mambo mema. Wanaume wengi hawakuwa wamepokea baraka ama kubariki wengine. Baada ya kusikiliza ujumbe wa Richard na kukisoma kitabu hiki, walipokea Baraka kuu na kuwawezesha kubariki wengine kwa jina la Baba, la Mwana na Roho Mtakatifu.

Napendekeza Richard pamoja na kitabu hiki cha 'Mastaajabu ya Nguvu za Kubariki' kama njia ya

kuachilia utele wa baraka ya Mungu katika familia zetu, jamii na hata taifa letu.

**Paul Subritzky**
National Director, Promise Keepers
Auckland, Nyuzilandi

# UTANGULIZI

Kila mmoja anapenda kusikia habari za kusisimua – na hata ni bora unapopata kulisema!

Nilipogundua thamani ya kutoa baraka, ilikuwa kama nilikuwa yule mtu katika Bibilia aliyegundua hazina katika shamba. Kwa shauku nilimshirikisha Pasta Geoff Wiklund katika fikira na niliyoyapitia ali-niomba niongee kwa wanaume wa kanisa lake katika kongamano mnamo February 2015. Walivutiwa sana wakataka kanisa lote liusikie ujumbe huo.

Nilipoongea katika kanisa, ilitokea kwamba Reverend Brian France, wa Charisma Ministries, na Paul Subritzky, wa Promise Keepers NZ, walikuwa wanahudhuria siku hiyo. Matokeo yake yalikuwa kuwasilisha ule ujumbe katika kule Charisma katika New Zealand na katika Fiji, na kwa wanaume katika Promise Keepers vilevile. Wengi waliupokea na mara wakaanza kuuweka katika vitendo kwa matokeo bora

sana. Baadhi wakatoa maoni hawakuwa wamewahi awali kusikia mafunzo kuhusu hali hii ya Ufalme wa Mungu.

Uchungaji wa kubariki ulionekana kuongezeka haraka. (Je, Mungu hasemi, 'Kipawa cha mtu kita-mfanyizia nafasi'?) Kuelekea mwisho wa 2015, niliandamana na Pasta Geoff hadi Kenya na Uganda. Alikuwa anawahudumia mamia ya mapasta wakihudhuria Kongamano la Majemedari. Hili lilikuwa tukio la kila mwaka ambapo wawakilishi walitafuta msukumo na kuungwa mkono, na Geoff alihisi mafunzo yangu kuhusu kubariki yangekuwa ya usaidizi kwao. Na lilitokea kuwa hivyo. Si mapasta pekee, bali wahutubu wengine kutoka Amerika, Australia na Afrika Kusini walihisi ulikuwa ujumbe wa nguvu na wakanihimiza nifanye kitu kufikia hadhira kubwa zaidi.

Sikutaka kuanzisha na kuendeleza mfumo wa mtandao, wala kuandika kazi ya kina wakati ambapo zingine bora tayari zipo. Ujumbe wa kubariki ni mwepesi sana kutekelezwa kwa urahisi na sikutaka wepesi wake upotelee katika ugumu wa kutoeleweka ndipo hiki kitabu kidogo.

Nimedondoa manukuu kutoka *The Power of Blessing* na Kerry Kirkwood, *The Grace Outpouring: Becoming a People of Blessing* na Roy Godwin na Dave Roberts, *The Father's Blessing* na Frank Hammond, na *The Miracle and Power of Blessing* na Maurice Berquist. Nina hakika nimevuta na nimejifunza kutoka kwa watu wengine na vitabu vingine pia, lakini baada ya miaka, vyote vimeungana pamoja.

Kugundua nguvu za kubariki kutaendeleza hali timilifu ya kuishi kwa yeyote atakayefuatilia. Mimi hubariki watu wengi sana sasa – katika waumini na wasio waumini katika mikahawa na hata njiani. Nimewabariki mayatima, wahudumu wa makao ya mayatima, mhudumu wa kike wa ndege katika ndege, mashamba ya miti ya matunda, wanyama, vibeti, biashara na hali za kiafya. Nimekuwa na wanaume na wanawake wazima wakililia kifuani pangu ninapokuwa nimetangaza baraka ya baba kwao.

Ninapozungumza na waumini, nimegundua kuwa kusema 'Hebu nikubariki/biashara yako/ndoa yako n.k?' hakutishi sana kuliko kusema, 'Ninaweza kuku-

ombea?' Kwa hakika, hii njia rahisi iliyo na upendo, ilimfanya mmoja wa jamaa zangu kujua upendo na nguvu za wokovu za Yesu Kristo, baada ya kupingana kwa miaka kadha.

Mara nyingi sipati kushuhudia matokeo lakini nimeona ya kutosha kujua kwamba kubariki hubadili maisha na kumebadili yangu pia.

Ni tabia ya Mungu kubariki na; kama viume wal-ioumbwa kwa mfano wake; katika uasili wetu wa kiroho vilevile. Roho Mtakatifu anawasubiri watu wa Mungu wajitokeze katika imani na katika mamlaka kwamba Yesu Kristo aliwashindia, ili kugeuza maisha.

Nina hakika utapata hiki kijitabu kikiwa chenye usaidizi. Yesu hajatuacha dhaifu. Kunena baraka katika aina zote za hali ni neema ya kiroho iliyopuu-zwa inayoweza kugeuza dunia yako.

Furahia.
**Richard Brunton**

SEHEMU YA KWANZA:

# Kwa Nini Kubariki?

# UTAMBUZI

Mke wangu Nicole ni wa makedonia Mpya na kwa hivyo, kama inavyotarajiwa, hilo lilimaanisha nilihitaji nijifunze kuongea Kifaransa na nikae kwa kiasi cha muda katika mahali pake pa kuzaliwa, Noumea. Ingawa Makedonia Mpya kwa wingi ni nchi ya Kikatoliki, haikuchukua muda mrefu kutambua kwamba watu wengi bado walikuwa na uhusiano na 'upande wa giza', wakati uohuo wakiendelea na dini yao. Haikuwa mara chache kwa watu kumtembelea mtu anayewasiliana na mizimu, mbashiri, au guérisseur bila kufahamu kwamba walikuwa wanafuata ushauri wa uchawi.

Ninakumbuka mke wangu alinipeleka kumtembelea kijana mwanamke wa miaka ishirini ambaye alikuwa amepelekwa kwa mmoja wa 'waponyaji', lakini ambaye, punde tu baadaye, alikuwa ameishia katika makao ya wenye kichaa au huzuni. Ambavyo nilifahamu alikuwa Mkristo, niliyaamuru mapepo mabaya

yaliyokuwa yamemwingia kwenda, katika jina la Yesu Kristo. Padre wa Kikatoliki aliomba vilevile, na kati yetu, huyu msichana aliachiliwa huru na kuruhusiwa kuondoka katika taasisi hiyo si muda mrefu baadaye.

Wengine walikiri dini yao ya Katoliki na wangali wanaonyesha waziwazi sanamu au vyombo vilivyobuniwa vya miungu mingine. Alikuwepo mwanamume mmoja wa dini ya Budha niliyomkuta akiwa daima na matatizo ya tumbo. Siku moja nilimwambia kwamba niliamini kwamba iwapo angeondoa yule Budha mkubwa mnono ambaye alikuwa mbele ya nyumba yake – iliteketezwa yote usiku – matatizo yake ya tumbo yangeisha. Tena, baadhi ya vyombo vilivyobuniwa alivyokuwa amekusanya ilibidi viondoke. Alipinga vipi hivi vitu 'vilivyokufa' vingeweza kunifanya mgonjwa? Baada ya miezi fulani nilimwona tena na kumwuliza jinsi lilivyokuwa tumbo lake. Kidogo kwa aibu alijibu, 'Mwishowe nilikubali ushauri wako nikaondoa Budha. Tumbo langu ni sawa sasa.'

Wakati mwingine, niliombwa niende katika nyumba ya mwanamke aliyekuwa na saratani. Kabla nianze kuomba, nilipendekeza waondoe sanamu za Budha

katika sebule yao, ambacho mume wake aliifanya mara hiyo. Nilipokuwa nikivunja laana zimwondokee na kuamuru mapepo mabaya kuondoka katika jina la Yesu; alieleza ubaridi sana kama barafu ukienda juu mwilini mwake kutoka nyayoni na kuondoka kichwani.

Kwa hivyo, katika msingi huu, niliamua kutoa funzo kuhusu 'laana' kwa kikundi cha maombi mke wangu na mimi tulikuwa tumeanzisha katika chumba chetu cha Noumea. Mafunzo yalitokana na kazi halisi ya Derek Prince (Derek Prince alikuwa mwalimu maarufu wa Bibilia wa karne ya ishirini). Nilipokuwa natayarisha ujumbe wangu katika Kifaransa, nilijifunza neno lao la kulaani lilikuwa *malédiction* na neno lao la kubariki lilikuwa *bénédiction*. Maana za mashina ya maneno haya ni 'unenaji mbaya' na 'unenaji mzuri'.

Awali, nilipolinganisha kulaani na kubariki, kulaani kulionekana giza, kuzito na hatari, na kubariki kulione- kana kwepesi kabisa na kwema. Nilikuwa nimewahi awali kusikia mafunzo kuhusu laana, lakini kamwe si kuhusu kubariki- ambayo labda ilichangia ufahamu wangu.Tena nilikuwa sijawahi kusikia yey-

ote akimbariki mtu mwingine kwa dhamira halisi na athari. Kwa kweli kiasi cha Mkristo kubariki huenda iwe ni kusema, 'Akubariki', mtu fulani apigapo chafya au kuandika 'Baraka' mwishoni mwa barua au barua pepe – kama kwamba ilikuwa karibu desturi badala ya kitu kilichokusudiwa.

Baadaye, nilipoyafikiria maneno haya 'laana' na 'baraka' ilinitokea kwamba ikiwa 'unenaji mbaya' ulikuwa wenye nguvu, basi 'unenaji mzuri' mpaka uwe vilevile angaa wenye nguvu na, pamoja na Mungu yawezakana, wenye nguvu zaidi!

Ufunuo huu, pamoja na ufahamu mwingine ambao tutazungumzia baadaye, ulinielekeza katika mwendo wa kugundua nguvu za kubariki.

# UWEZO WA UNENAJI WETU

Bila kutaka kurudia yale vitabu vingi vizuri vimesema kuhusu uwezo wa maneno yetu, nataka nitoe muhtasari wa ninaloamini ni muhimu katika sehemu hii.

Tunajua kwamba:

> *Mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi na wale wanaoupenda watakula matunda yake. (Methali 18:21)*

Maneno yana uwezo mkubwa sana aidha chanya na za kujenga, ama hasi na za kubomoa. Kila wakati tunanena maneno (na hata kutumia sauti maalumu, ambayo huongeza maana katika maneno hayo), tunanena aidha uzima au mauti kwa hao watusikiao na kwetu wenyewe. Zaidi ya hayo, tunajua kwamba:

> *Kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake. Mtu mwema katika akiba njema hutoa mema, na mtu mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya. (Mathayo 12:34-35)*

Hivyo, kutoka katika moyo wa kukosoa ulimi wa kukosoa hunena; kutoka katika moyo wa kujiona mkamilifu, ulimi wa kuhukumu; moyo usio na shuk- rani; ulimi wa kunung'unika; na kadhalika. Vivyo hivyo, mioyo ya tamaa huzaa tunda linalolingana. Dunia imejaa unenaji hasi. Vyombo vya habari hutapika siku baada ya siku. Tabia ya wanadamu ikiwa jinsi ilivyo, tunaelekea kutonena vyema kwa watu na hali. Mara nyingi tunangoja mpaka watu wafe kabla kusema mambo mazuri kuwahusu. Kwa hali yoyote, ile akiba njema hutokeza nje ya mioyo ya upendo itakayonena kwa ulimi wa neema; kutoka katika mioyo ya amani, ulimi wa upatanisho; na kadhalika.

Maelezo, na wale 'wanayoipenda, watakula tunda lake' yanamaanisha tutavuna tunachopanda kiwe kizuri au kibaya Katika maneno mengine, utapata unachosema. Unaonaje kuhusu hilo?

Hii ni kweli kwa wanadamu wote, pasipo kujali kama wana imani ya Kikristo au la. Wakristo na wasio wakristo wote ni sawa katika kunena maneno ya uzima – kwa mfano, ama wanaweza kusema: 'mwanangu, umejenga kijumba kizuri cha nguvu. Hata unaweza kuwa mjenzi hodari au mchoraji wa nyumba siku moja. Hongera'.

Hata hivyo, mkristo aliyeokoka ana moyo mpya. Bibilia inatwambia kwamba sisi ni 'viumbe vipya' (2 Wakorintho 5:17). Kwa hivyo, kama Wakristo, tuwe tukifanya sana unenaji mzuri kidogo mbaya. Tunaweza kuteleza kwa urahisi katika uhasi tusipojihadhari kuchunga mioyo na maneno yetu. Mara utakapoanza kuyatafakari haya kwa ufahamu, utashangaa jinsi mara nyingi Wakristo – hata pasipo kujua – hujilaani na kuwalaani wengine. Mengine kuhusu hilo baadaye.

# KUTOKA KATIKA UNENAJI MZURI HADI KUBARIKI: WITO WETU

Kama Wakristo, na maisha ya Bwana Yesu yakitiririka kutokana nasi, tunaweza kwenda zaidi ya unenaji mwema tu – tunaweza kunena na kusababisha baraka kwa watu au hali na hasa tumeitwa tufanye hivyo pengine kubariki ndio wito wetu mkubwa. Soma ifuatayo:

> *Muwe wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitivu, wanyenyekevu, watu wasiolipa baya kwa baya au laumu kwa laumu, bali wenye kubariki; kwa sababu hayo ndiyo mli-yoitiwa ili mrithi baraka. (Waraka wa Kwanza wa Petro 3:8,9)*

Tumeitwa kubariki na kupokea baraka.

Kitu cha kwanza alichonena Mungu kwa Adamu na Hawa kili- kuwa baraka:

> *Mungu akawabariki, Mungu akawambia: 'Zaeni, mkaongezeke; mkajaze nchi na kuitiisha…' (Mwanzo 1:28.)*

Mungu aliwabariki ili wakaweze kuongezeka. Baraka ni sifa ya (kiasili ya) Mungu – ni kitu afanyacho! Na kama Mungu – na kutoka kwa Mungu – na sisi pia tuna mamlaka na uwezo wa kuwabariki wengine.

Yesu alibariki. Kitu cha mwisho alichokifanya, hata alipokuwa karibu kupaa mbinguni kilikuwa kuwabariki wanafunzi wake.

> *Akawaongoza mpaka Bethania, Akainua mikono Yake Akawabariki. Ikawa katika kuwabariki Alijitenga nao, Akachukuliwa juu mbinguni. (Luka 24:50,51)*

Yesu ni kielezo chetu. Akisema kwamba tufanye vitu sawa na alivyofanya, katika jina lake. Tumekusudiwa na Mungu tubariki.

# BARAKA YA KIKRISTO NI NINI?

Katika Agano la Kale, neno 'baraka' ni neno la Kiebrania baraka. Hili maana yake; 'kunena kusudio la Mungu tu'.

Katika Agano Jipya 'baraka' ni neno la Kigiriki, *eulogia* kutokana nalo tunapata neno *eulogy* taabin (maneno ya kusifu). Kwa hivyo; katika matumizi, maana yake ni kunena 'wema kuhusu' au 'nena kusudio na fadhila ya Mungu' kwa mtu.

Hiyo ndiyo fasili ya kubariki nitakayotumia katika kitabu hiki. Kubariki ni kunena makusudio au fadhila ya Mungu kwa mtu au hali fulani.

Mungu, kwa kiwango kikubwa, katika hekima yake ameamua kuwekea mpaka kazi yake duniani hadi Anachoweza kutimiza kupitia kwa watu wake. Hivi ndivyo aletavyo ufalme wake katika dunia. Kufuatana na hayo, anataka tubariki kwa niaba yake. Kwa

hivyo, kama Mkristo ninaweza kunena makusudio na fadh- ila kwa mtu au hali fulani katika jina la Yesu. Nikifanya hivyo kwa imani na upendo basi nina uwezo wa mbinguni katika ninalosema, na ninaweza kutara- jia Mungu atachukua hatua kubadilisha vitu kutoka vilipo, hadi atakapo viwe. Ninapombariki mtu kwa makusudi, kwa upendo na imani ninamwezesha Mungu kuchochea mipango yake kwa huyo mtu.

Kwa upande mwingine, mtu anaweza kwa makusudi, au kwa kawaida kutokuwa mwangalifu, kunena makusudio ya shetani kwa mtu, au hata kwake mwenyewe, ambako basi huziwezesha nguvu za kishetani kuchochea mipango yazo kwa mtu huyo – yaani, kuiba na kuharibu. Lakini Mungu asifiwe,

> *'Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia' (1 Yohana 4:4).*

Bila shaka ni moyo wa Mungu kubariki – hasa bila shaka hali yake! Hamu ya Mungu kubariki ni ya kupita kiasi vibaya mno. Hakipo kinachoweza kumsimamisha. Amekusudia kubariki wanadamu. Hamu yake ni kwamba Yesu Atakuwa na ndugu na dada wengi. Hao

ni sisi! Tena, ingawa bila shaka ni moyo wa Mungu kubariki wanadamu, ana hamu hata zaidi kwamba watu wake watabarikiana.

Tunapobariki katika jina la Yesu, Roho Mtakatifu huja kwa sababu tunaakisi kitu ambacho Baba Anafanya tunanena maneno ambayo Baba hutamani yasemwe. Nina staajabu kila wakati jinsi ukweli huu ulivyo. Ninapombariki mtu Roho Mtakatifu anahusika – Humgusa mtu mwingine, upendo unaachiliwa na vitu vinabadilika. Mara nyingi watu hunikumbatia baadaye au hulia na kusema, 'Hujui jinsi ulivyokuja wakati ufaao na ulivyokuwa wenye nguvu', au 'Hujui jinsi nilivyoutaka sana'.

Lakini kuna kitu muhimu sana cha kutilia maanani: tunabariki kutoka mahali pa urafiki mkubwa na Mungu kutokana na uwepo wake. Ukaribu wetu kiroho na Mungu ni muhimu kabisa. Maneno yetu ni maneno Yake na yana upako wa uwezo kukamilisha makusudio yake kwa mtu huyo au hali hiyo. Lakini wacha tuunge mkono kidogo…

# MAMLAKA YETU YA KIROHO

Katika Agano la kale, makuhani walikuwa wawe wakiomba kwa watu na kutamka baraka kwao.

> *Hivi ndivyo mtakavyowabarikia wana wa Israel. Mtawaambia: Bwana akubarikie na kukulinda*
>
> *Bwana Akuangazie nuru za uso Wake na kukufadhili. Bwana Auinulie uso wake, na kukupa amani.*
>
> *Ndivyo watakavyoweka jina Langu juu ya wana wa Israel, na Nitawabarikia. (Hesabu 6:23-27)*

Katika agano Jipya, sisi kama Wakristo tumeitwa:

> *…mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa miliki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili Zake Yeye Aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu. (Waraka wa Kwanza wa Petro 2:9)*

Na Yesu

> *…ametufanya kuwa wafalme, na makuhani kwa Mungu Wake na Baba. (Ufunuo 1:6)*

Wakati fulani uliopita, nilikuwa nimekaa katika Ouen Toro, mahali pa kutazamia katika Noumea, nikitafuta ujumbe wa kuletea kikundi cha maombi. Nilihisi Mungu akisema, 'Hujui wewe ni nani.' Basi baada ya miezi fulani: 'Kama ungejua mamlaka uliyo nayo katika Yesu Kristo ungebadilisha dunia.' Jumbe hizi zote zilikuwa kwa makundi maalumu ya watu lakini nilitambua baadaye zilikuwa kwangu pia.

Nafikiri kwa jumla inajulikana katika jamii za Kikristo kwamba kunena moja kwa moja kwa mgonjwa au hali 'mlima' (Mariko 11:23) na kuamuru uponyaji kuna nguvu zaidi ya kumwuliza Mungu afanye (Mathayo 10:8; Mariko 16:17-18). Huu kwa hakika umekuwa uzoefu wangu na uzoefu wa watu wengi maarufu na waheshimiwa wanaofanya huduma ya kufaulu katika uponyaji na ukombozi. Ninaamini Yesu anasema kwa ukweli. 'Wewe ponya wangojwa (katika jina Langu). Si kazi yangu, ni kazi yako. Wewe fanya hivyo.'

Mungu anataka kuponya na anataka kufanya hivyo kupitia kwetu sisi. Mungu anataka kukomboa na anataka kufanya hivyo kupitia kwetu sisi. Mungu anataka kubariki na anataka kufanya hivyo kupitia kwetu sisi. Tunaweza kumwuliza Mungu abariki, au tunaweza kubariki katika jina la Yesu.

Miaka fulani iliyopita, ninakumbuka nikichukua muda kwenda kazini mapema kubariki biashara yangu. Nilianza na 'Mungu, bariki Colmar Brunton.' Ikawa bila ladha. Basi nikabadilisha kwa woga kidogo mwanzoni kutoka 'Mungu bariki Colmar Brunton' hadi:

*Colmar Brunton, ninakubariki katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Ninakubariki katika Auckland, na ninakubariki katika Wellington, na ninakubariki katika majimbo.*
*Ninabariki katika kazi na ninakubariki nyumbani.*
*Ninaachilia Ufalme wa Mungu mahali hapa.*
*Njoo Roho Mtakatifu, Unakaribishwa hapa.*
*Ninaachilia upendo na furaha na amani na uvumilivu na ukarimu na wema na upole na uaminifu na kujizuia nafsi na umoja katika jina la Yesu, ninaachilia mawazo kutoka katika Ufalme*

*wa Mungu ambayo yataweza kusaidia wateja wetu kufaulu na kuifanya dunia mahali bora. Ninaachilia fadhila katika soko la wateja. Nanaachili fadhila katika soko la uajiri. Ninaachililia maono yetu: 'Biashara Bora, Dunia Bora'. Katika jina la Yesu, amina.*

Jinsi nilivyohisi nikiongozwa nilikuwa nikifanya ishara ya msalaba katika langa letu na kiroho kutumia ulinzi wa damu ya Yesu katika biashara yetu.

Tangu muda mfupi sana nilipobadili kutoka 'Mungu bariki Colmar Brunton' hadi 'Ninabariki Colmar Brunton katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu', mafuta ya upako wa Mungu yaliniangukia – nilikuwa nahisi furaha na uthibitisho wa Mungu. Ilikuwa kama Alikuwa Akisema, 'Umepata mwana; hicho ndicho ninachotaka ufanye.' Ingawa mpaka niwe nimefanya hivi sasa mara ya mamia, daima nimehisi furaha ya Mungu ikiwemo. Na matokeo? Mazingira katika office yalibadilika na yalibadilika haraka hadi kiwango cha watu kuzungumzia waziwazi na kushangaa sababu ya vitu kuwa hivyo. Kwa kweli ilikuwa ya kushangaza. Kubariki kunaweza kwa kweli kubadilisha dunia yetu.

Lakini sikuachia hapo. Asubuhi, ofisi ikiwa tupu, nilipokijia kiti cha mtu aliyehitaji busara kwa hali maalumu, niliwabariki, nikiweka mikono juu ya kiti, nikiamini kwamba upako wa kukamilisha kule kubariki ungepitia katika kitambaa cha kiti na hivyo hadi kwa mtu aliyekikalia (Matendo 19:12). Kila nili-potambua mahitaji maalumu waliyokuwa nayo, ningebariki katika njia hiyo.

Hasa nilimkumbuka mtu aliyezoea kukufuru yaani, alitumia jina la Mungu kama mzaha. Asubuhi moja niliwekelea kiti chake mikono, nikifunga roho ya kukufuru, katika jina la Yesu. Nilifanya hivyo mara kadhaa, lakini mwishowe pepo mbaya aliyehusika alilazimika kupigia goti uwezo mkubwa zaidi na kukufukuru kukatoweka katika msamiati wa mtu huyo mahali pa kazi.

Pia ninakumbuka mwanamume akinijia kwa ombi, akitaka Mungu amwondoe mahali pake pa kazi kwa sababu kila mtu pale alikuwa akikuufuru. Nilichukua msimamo tofauti: huyu mwanamume alikuwa pale abariki mahali pake pa kazi na abadilishe mazingira! Tunaweza kubadilisha dunia yetu.

Nimechukua msimamo kwamba ingawa 'Mungu anatamani kubariki wanadamu, anatamani hata zaidi kwetu – Watu wake, watoto wadogo Wake – kubariki wanadamu. Una mamlaka ya kiroho. Wewe bariki.

Baba yetu wa mbinguni Anataka tushiriki, tufanye kazi kwa ushirika, pamoja Naye katika kazi Yake ya kuokoa. Tunaweza kubariki wanadamu kwa upon-yaji na ukombozi lakini tunaweza pia kubariki kwa maneno yetu. Sisi ni watu Mungu awatumiao kubariki dunia. Ni upendeleo na uwajibikaji ulioje!

Kwa hivyo, kwangu mimi kubariki ni kunena makusudi ya Mungu kwa maisha ya watu au hali kwa upendo, uangalifu, makusudi, kwa mamlaka na uwezo, kutoka kwa roho yetu iliyojaa Roho Mtakatifu. Kwa maelezo rahisi, kubariki ni kutenda katika imani kwa kutamka kusudi la Mungu kwa mtu au hali. Tunapotamka kusudi la Mungu, tunaachilia uwezo wake kubadili-sha vitu kutoka vilipo hadi anakotaka viwe.

Na ukumbuke – tunabarikiwa kwa sababu tunabariki.

SEHEMU YA PILI:

# Namna ya Kukifanya

# BAADHI YA KANUNI MUHIMU

**Fanya kinywa chako kunena mema**

> *Katika kinywa kile kile hutoka baraka na laana. Ndugu zangu, haifai mambo haya kuwa hivyo (Yakobo 3:10 NLB)*

> *Nawe ukitoa kilicho cha thamani katika kilicho kibovu, utakuwa kama kinywa changu. (Yeremai 15:19b, RSV)*

Ukitaka kunena nia ya Mungu kwa watu, basi itakubidi uwache kunena mambo yasiyofaa.

**Uliza Roho Mtakatifu utakachosema**

Chochea roho yako (kwa kuabudu ama kunena na ndimi) uliza Roho Mtakatifu akusaidie uweze kuhisi

upendo wa Baba kwa unayetaka kumbariki. Omba jinsi hii:

> *Baba, wapenda yapi yasemwe? Tafadhali nipe neno la baraka kwa mtu huyu. Ninawezaje kumhimiza au kumfariji?*

**Baraka ilivyo tofauti na uombezi**

Watu wengi sana huona kwamba ni vigumu kweli kunena baraka. Siku zote huanza 'kufanya uombezi' wakimwuliza Baba kubariki. Ingawa hili ni jambo zuri kufanya, baraka ikinenwa hivi hasa ni sala, na ni muhimu kujua tofauti. Kunena au kutamka baraka hakuchukui mahali pa sala na uombezi lakini ni rafiki kwao kawaida pamoja.

Waandishi Roy Godwin na Dave Roberts katika kitabu chao *The Grace Outpouring* wanaeleza hili vizuri sana:

> *Tunapobariki, tunamtazama mtu machoni (ikiwa hiyo ndiyo hali) na kunena moja kwa moja kwake. Kwa mfano, tunaweza kusema kitu, kama 'Ninakubariki katika jina la Bwana,*

*kwamba neema ya Bwana Yesu iwe kwako. Ninakubariki katika jina Lake kwamba mapenzi ya Baba yakaweze kukuzingira na kukujaza; kwamba uweze kujua katika ndani kabisa ya nafsi yako hasa jinsi anavyokukubali kabisa na kikamilifu na kukufurahia'*

*Angalia kiwakilishi nafsi 'Ni'. Ni mimi ninayetamka baraka katika jina la Yesu kwa mtu moja kwa moja. Sijamwomba Mungu baraka lakini nimenena baraka nikitumia mamlaka atupayo Yesu kutamka baraka kwa watu ili akaweze kuja na kuwabariki.*

**Usihukumu**

Usitoe hukumu iwapo mtu anastahili baraka au hastahili. Baraka za kweli, zilizonenwa juu ya mtu au kitu, huelezea jinsi Mungu anavyowatazama. Mtazamo wa Mungu sio vile mtu anavyoonekana wakati huo, ila anavyotakikana kuwa.

Kwa mfano, Mungu alimwita Gideoni, 'Shujaa mkuu' (Waamuzi 6:12b) lakini wakati ambapo alikuwa mtu

bure! Yesu akamwita Petro, 'Mwamba' (Mathayo 16:18) kabla hajapata 'mabega' ya kuwabeba wengine. Tunasoma zaidi kuwa, 'Mungu mwenye kuwahuisha wafu, ayatajaye yale yasiyokuweko kana kwamba yamekuweko' (Warumi 4:17b). Tukiyajua haya, yatatuondolea ile tabia ya 'Kuhumu', iwapo mtu fulani anastahili baraka.

Wale watu tunaowafikiria kuwa hawastahili kubarikiwa, ndio wanastahili kubarikiwa zaidi. Watu wabarikio wasiostahili kubarikiwa hupokea baraka kuu.

**Mfano wa kuelezea**

Jaribu kudhania kuwa kuna mtu aitwaye Fred ambaye ana shida ya ulevi. Mke wake hafurahishwi na jambo hili, kwa hivyo anaweza kuomba jinsi hii: '*Mungu bariki Fred, msaidie aache kulewa na anisikize mimi*'. Lakini yangekuwa na nguvu zaidi kama angeomba hivi:

> *Fred, nakubariki katika jina la Yesu. Mpango wa Mungu juu ya maisha yako na ukatimie. Na uwe*

*mtu, bwana na baba ambaye Mungu amekusudia uwe. Ninakubariki na uhuru kutokana na kulevya. Ninakubariki na amani ya Kristo.*

Baraka ile ya kwanza inawakilisha shida ile kwa Mungu. Haichukui juhudi yeyote-ni dhaifu. Pia inahukumu na kuangazia dhambi za Fred.

Baraka ile ya pili inaitaji fikira zaidi na upendo zaidi. Haihukumu na inaangazia uweza wa Fred badala ya hali yake ya wakati huo. Hivi karibuni nilisikia mtu akisema yakuwa Shetani anajua majina yetu na uweza wetu lakini anatuita kwa dhambi zetu, ila Mungu anajua dhambi zetu lakini anatuita kwa majina yetu halisi na uweza wetu. Baraka hii ya pili iko zaidi katika mpango na makusudi ya Mungu. Inaangazia moyo wa Mungu wa ukombozi. Kumbuka, Mungu anampenda Fred.

# HALI TOFAUTI TOFAUTI TUNAZO WEZA KUKABILI

Mimi ni mwanafunzi wa kubariki. Nilipoanza sikujua jinsi ya kubariki na sikuweza kupata mengi ya kunisaidia. Kwa kweli nilianza haraka kutambua kwamba kuna hali nyingi tofauti, kwa hivyo nakutolea mapendekezo yanayofuata. Unaweza kuyabadilisha kulingana na mahitaji ya hali maalumu na kufuatana na kile unachoamini Roho Mtakatifu anataka kusema. Hili litaitaji mazoezi lakini lina thamani Fulani.

**Kubariki wale ambao hukushutumu au hukulaani**
Miaka mingi iliyopita, mwajiriwa (wakike) aliyekuwa amejiuzulu punde alikuja kwangu kwa kahawa na kusema kwa heri. Imani zake zilikuwa kulingana na mtazamo wa kisasa 'wema wa ndani', naye ale kama hilo. Wakati wa mazungumzo, alisema kwamba kampuni mbili za mwisho alizokuwa amezifanyia kazi, na kuondoka, zilikuwa baadaye zimefilisika.

Sikuwa nimekuwa Mkristo kwa muda mrefu wakati huo, lakini, nilitambua maneno yake yalikuwa laana ikionekana kushuka. Nilihisi sekunde chache za woga na halafu, katika akili nilikataa kuikubali. Lakini sikwenda hatua ya ziada ya kumbariki. Baada ya kumtaka idhini ya kuomba kilichokuwa katika moyo wangu, ningeweza kusema kitu kama:

> *Debora (si jina lake kweli), ninafunga ushawishi wa uchawi katika maisha yako. Ninakubariki katika jina la Yesu. Ninatamka wema wa Mungu kwako. Makusudio ya Mungu kwa maisha yako yapate kufika. Ninabariki vipawa vyako, vibarikie mwajiri wako wa siku zijazo na kuleta utukufu wa Mungu. Uweze kuwa mwanamke mzuri sana wa Mungu ambaye anakukusudia uwe. Katika jina la Yesu, amina.*

**Kubariki waliokujeruhi au kukukataa**

Wakati mmoja nilimwombea mwanamke ambaye aliuwa aking'ang'ana kimawazo na kifedha baada ya mume wake kumwacha. Nikamuuliza kama angeweza kumsamehe mumewe. Kwa kweli ilikuwa ni

vigumu lakini kwa wema wake alifanya hivyo. Halafu nikamuuliza kama angeweza kumbariki mume wake. Alishtuka kidogo lakini alikuwa mwepesi wa kutaka kujaribu. Hata kama mume wake hakuwako, nilimwongoza kusema hivi:

> *Ninakubariki wewe mume wangu. Mipango ya Mungu juu ya maisha yako na ndoa yetu iweze kuzalisha matunda. Uweze kuwa mwanamume, mume na baba ambaye Mungu amekusudia uwe. Neema ya Bwana na kibali chake iwe nawe. Katika jina la Yesu. Amina.*

Hili halikuwa jambo sawa la kuanzia, lakini aligusa moyo wa Baba na upako wa Mungu ukashuka. Sote tulikuwa tunalia huku Roho wa Bwana akimhudumia. Na ninaamini ilikuwa vile hata kwa mume wake. Njia za Mungu si kama zetu.

Kubariki katika hali hizi zote kunahitaji ujasiri, ukuu, usawa na kuchukua mfano wa Kristo.

Kubariki wasiostahili ndio moyo wa Mungu- hapo ndipo Mungu ana umaarufu. Tilia maanani yule

mwizi aliyesulubiwa pamoja na Yesu au mwanamke mwasherati aliyefumaniwa.

Je, wewe na mimi?

Baraka 'si ya kilimwengu' na siyo kitu ambacho baadhi ya watu walio katika hali ya kujeruhiwa huhisi kufanya. Lakini ni njia ya Mungu, na yaweza kuponya anayebariki na hata anayepokea baraka. Hii huondoa sumu za machungu, kulipiza kisasi, kutofurahiswa na hasira, ambayo yaweza kudhuru mwili na kufupisha maisha.

Hii hapa ni barua pepe niliyopokea juzi kutoka kwa Denis:

> *Karibu miezi mitatu iliyopita nilikuwa nikizungumza na kakangu kwa simu. Huwa hatuwasiliani sana kwa sababu yeye huishi na kufanya kazi mji mwingine. Tulipokua karibu kumaliza mazungumzo yetu ya kirafiki nilimuuliza kama angeniruhusu kubariki biashara aliyokuwa akiendesha na mukewe. Hakuitikia vizuri. Alijawa na ujeuri na kutamka jambo lililonikasirisha sana, nikawa nina*

*shangaa kama urafiki wetu iwapo ulikuwa umeharibika milele. Hata hivyo, katika siku na majuma yaliyofuatia, nikiwa katika harakati zangu za kila siku, nilitumia kanuni za mastaajabu ya nguvu za kubariki kunena kibali cha Mungu katika biashara ya ndugu yangu. Wakati mwingine nilifanya havyo mara mbili hadi mara tatu kwa siku. Miezi mitatu baadaye, siku moja kabla ya Krismasi, kakangu alinipigia simu kana kwamba hakukuwa na cho chote kilichotendeka kati yetu. Nilishangazwa sana na urafiki wake, hata hapakuwa na maonevu kati yetu kabisa. Mastaajabu ya nguvu za kubariki katika hali tusiyoweza kuizuia hufanya kazi kabisa… Bwana asifiwe.*

**Kubariki wale ambao wamekuchokeza**

Mojawapo ya vitu vinavyokasirisha sana kwa baadhi yetu ni watu wafanyapo vitu vyenye ubinafsi, visivyojali wengine au kudanganya waziwazi katika wendaji wa watu na magari barabarani. Hili hufanyika kila wakati. Maneno kadhaa yasiyo ya Kikristo yanaweza kurukia akili na kutoka katika midomo yao katika

muda si muda. Hili litokeapo tunamlaani mtu ambaye aliumbwa na Mungu na ambaye Mungu anampenda. Mungu anaweza kumtetea vizuri sana mtu huyo.

Wakati mwingine hili litokeapo, jaribu kumbariki yule dereva mwingine, badala ya kuongea maneno ya hasira:

> *Ninambariki yule mwanamume chipukizi aliyekata ndani kwangu (alidanganya katika foleni). Ninatamka upendo Wako kwake Bwana. Ninauachilia wema Wako kwake na makusudio Yako yote kwa maisha yake. Ninambariki huyu mwanamume chipukizi na ninauita uwezo wake. Afike nyumbani salama na baraka kwa jamaa yake katika jina la Yesu, amina!*

Au kwa wepesi:

> *Baba, ninambariki dereva wa gari hilo katika jina la Yesu. Upendo wako ukamuandame, umpite na hata kumshika!*

Mmoja wa wasomaji wa kitabu changu alitoa maoni ya kuvutia:

*Kile nilichotambua ni kwamba baraka zimenibadilisha. Siwezi kuwabariki watu ambao wameniudhi, kwa mfano, halafu ninene-au hata niwaze- mawazo maovu juu yao. Hayo yatakua makosa. Badala yake natazamia kupata matokeo mazuri kutokana na baraka hizi… – Jilian.*

Wakati mmoja nilikua na rafiki aliyeitwa John ambaye alinialika kwa maombi kuhusu mzozo wa jamaa uliohusu urithi. Mzozo ulikuwa unajikokota na kuendelea kuwa wa kutokufurahisha. Nilipendekeza badala ya kuomba tuibariki hali hiyo.

*Tunabariki hali hii ya mzozo kuhusu urithi huu katika jina la Yesu. Tunapinga utengano, ushindani na ugomvi na kuachilia haki na kutopendelea na upatanisho. Tunapobariki hali hii, tunaweka kando mawazo yetu sisi wenyewe na tama na kuachilia Mungu achochee makusudio yake kwa ugawanyaji wa urithi katika jina la Yesu, amina.*

Katika siku mbilitatu jambo hilo lilisuluhishwa kirafii. Kubariki kunaweza kweli kubadilisha dunia yetu.

# KUJIBARIKI BADALA YA KUJILAANI

**Kutambua na kuvunja laana**

Mawazo haya ni ya kawaida vipi: 'Nina sura mbaya, mimi ni mjinga, mimi siwezi, mimi ni bozi, hakuna anipendaye, Mungu hangeweza kunitumia, mimi ni mtenda dhambi…'? Upo uongo mwingi ambao shetani hutufanya tuamini.

Nina rafiki ambaye hufanya hivi kila wakati na huni-huzunisha. 'Oo, we msichana mjinga, Rosa (si jina lake kweli). Umevuruga tena. Huwezi kufanya chochote sawasawa…'

Usirudie wala usikubali hizi laana! Badala yake, jibariki.

Ninakumbuka hali maalumu ya kundi la maombi. Nilitambua roho ya kutokuwa na thamani juu ya bibi ambaye alikuwa amekuja kuombewa. Katika hali ya

kuomba, alisema, 'Mimi ni mpumbavu'. Nilimuuliza alikolisikia lile. Aliniambia wazazi wake walisema kwake. Sikitiko lililoje… na nikawaida sana.

Nilimwongoza kulingana na maneno haya:

> *Katika jina la Yesu, ninawasamehe wazazi wangu. Ninajisamehe. Ninayavunja maneno ya wazazi wangu na ninajinenea. Nina akili ya Kristo. Mimi ni mwerevu.*

Mara moja tulizifukuza roho za kukataliwa na kutokuwa na thamani na halafu nilimbariki na nikanena kwake kwamba alikuwa binti mfalme wa Mungu, kwamba alikuwa mwenye thamani kwake, kwamba Mungu alikuwa anaenda kumtumia kuwa- bariki wengine, kuleta uponyaji wa kichaa na matumaini kwa wengine. Nilimbariki kwa ujasiri.

Polepole baraka hii ilimwingia. Alianza kung'ara. Wiki iliyofuata, alisimulia jinsi ilivyokuwa imemfanyia vizuri. Kwa kweli tunaweza kubabilisha dunia yetu.

Mtu yeyote anaweza kufanya hili. Bibilia imejaa maku-

sudio ya Mungu kwa watu na tunaweza kutamka makusudio haya kwao.

Ninapenda kueleza mfano mwingine. Nilimwombea bibi ambaye alikuwa na maumivu ya tumbo. Nilipokuwa ninaomba, Roho Mtakatifu alimwangukia na alijikunja mashetani yalipokuwa yakimwondoka. Kila kitu kilikuwa sawa kwa siku chache na halafu maumivu yakarudi, 'Kwa nini, Bwana' Aliuliza. Alihisi Roho Mtakatifu akimkumbusha kwamba wakati fulani kabla, alipokuwa katika mkutano mtu alikuwa amemwambia ahakikishe amepika kuku vizuri au watu wangekuwa wagonjwa. Alijibu hakutaka awe mgonjwa kwa siku chache zilizofuata (kipindi cha mkutano) lakini kwamba haingejalisha baada yake. Alilazimika aivunje nguvu ya hayo maneno ya ovy-oovyo, na halafu mara moja alipata tena uponyaji wake wa kujibariki mdomo.

**Kujibariki mdomo**

*Ninaubariki mdomo wangu kunena yaliyo na thamani nasi yasiyo na thamani na kuwa sawa*

*na mdomo wa Bwana. (Kutokana na Yeremiah 15:19)*

Miujiza mingi ya Yesu ilitimizwa kwa kunena tu. Kwa mfano, *'Enenda; mwanao yu hai'* (Yohana 4:50). Nataka hilo. Hiyo ndiyo maana mimi hubariki mdomo na kulinda kitokacho ndani yake.

Mke wangu na mimi tulikuwa wakati mmoja tunaishi hotelini katika Noumea. Tuliweza kusikia mtoto mchanga akilialia karibu bila kukoma usiku kucha. Baada ya siku mbilitatu za jambo hili, mke wangu alienda hadi roshani inayopakana na kumwuliza mama lililokuwa baya. Yule mwanamke hakujua lakini alisema daktari alikuwa amempa mtoto mchanga huyo hadi kipimo cha tatu cha dawa ya kia vijasumu na bila kilichofanya kazi. Mke wangu alimuuliza kama ningemwombea yule mtoto mchanga na alikubali, ingawa kwa kushuku. Kwa hivyo, katika Kifaransa changu cha kawaida kabisa, nilimwombea yule mtoto mchanga na kunena katika imani kwa yule mtoto, kwamba angelala kama mtoto mchanga (angelala fofofo). Na alilala hivyo.

**Kujibariki fikira**

Mimi husema mara kwa mara,

> *Ninabariki fikira zangu; nina fikira za Kristo. Kwa hivyo ninafikiri mawazo yake. Fikira yangu iwe mahali patakatifu ambapo Roho Mtakatifu anafurahia kuishi, ninapokea maneno ya maarifa na hekima na ufunuo.*

Mara nyingi, mimi hupambana na utakatifu wa fikira zangu na ninapata kusaidia. Pia mimi hubariki ubunifu wangu kwamba utumike kwa wema na si kwa uovu. Nilikuwa ninapata shida na ubunifu wangu siku nyingine – ulikuwa unachanganyiwa mahali mbalim- bali sikutaka kwenda – na Mungu Alinishawishi *'Ona katika ubunifu wako Yesu Akifanya miujiza yake… halafu jione wewe ukiifanya.'* Nimepata kuna nguvu zaidi katika kufikiria kitu kizuri (Wafilipi 4:8) baada ya kufukiria kutofikiria kitu! Na kubariki mawazo na ubunifu wako mwenyewe husaidia sana katika kufanikisha lengo la utakatifu.

Mara nyingine nilipokuwa ninasikia kushushwa

kuhusu kushindwa katika mawazo yangu,maneno ya zaburi ya kale ilibubujika ndani ya moyo wangu:

*Uwe maono yangu, ewe Bwana wa moyo wangu.*
*Yote iwe bure kwangu ila wewe tu*
*Wewe u mawazo yangu njema mchana au usiku*
*Kuamuka au kulala. Uwepo wako u nuru yangu.*

**Kujibariki miili yetu**

Unajua vizuri sana mstari: *'Moyo uliochangamka ni dawa nzuri'* (Methali 17:22). Bibilia inasema kwamba miili yetu hujibu maneno na fikira chanya (za kujenga).

*Ninabariki mwili wangu. Leo ninavunjilia mbali udhaifu. Nina bariki uzima wangu kimaumbile.*

Wakati mmoja nilitazama video kuhusu mwanaume aliyekuwa na tatizo baya la moyo. Njia yake ya kando ilikuwa imeziba. Alikuwa amebariki ateri zake kwa karibu miezi mitatu, akizitamka ziumbwe ziwe za kuhofisha na kustaajabisha. Kurudi kwa daktari, iligunduliwa kwamba kimuujiza alikuwa na njia ya kando mpya!

Nilifikiri ningeweza kujaribu hili kwa ngozi zangu. Nilikuwa na tatizo la uharibifu wa jua tangu ujana wangu. Sasa katika uzee wangu, vitu vidogo vingemea katika mabega na mgongo wangu, vikataka kugandishwa kwa barafu kila miezi michache. Niliamua kubariki ngozi yangu. Mwanzoni nilibariki tu katika jina la Yesu. Lakini nilikuwa nimesoma kitu kuhusu hali ya ngozi ambacho kilinifanya nibadilishe mtazamo wangu. Nilikuwa nimetambua kwamba, ingawa nimefunikwa nayo, sikujua mengi kuhusu kiungo kikubwa zaidi katika mwili wangu. Nilikuwa nimezungumza kuihusu, lakini sikuwa nimeizungumzia. Na nina shaka nilikuwa nimesema chochote kizuri kuihusu – badala yake nililalamika. Nilikuwa nisiye na shukurani.

Ngozi inastaajabisha. Ni mfumo wa kusafisha hewa na kuondoa maji machafu na takataka. Hukingia mwili vijidudu vinavyoshambulia na hujiponya yenyewe. Hufunika na kulinda sehemu zote za ndani na hufanya hivyo vizuri sana.

*Shukurani Mungu kwa ngozi – mikunjo na vyote. Bariki wewe, ngozi.*

Baada ya miezi kadha ya kubariki kwa aina hii, ngozi yangu sasa karibu ipone, lakini ufunguo ulikuwa nilipoanza kufurahi na kuwa mwenye shukurani kwayo. Imeumbwa vya kuhofisha na kustaajabisha. Funzo la kweli hasa. Kulalamika hufukuza Ufalme wa Mungu, shukurani humvutia.

Hapa upo ushuhuda kutoka kwa rafiki yangu, David Goodman:

> *Miezi kadhaa iliyopita nilimsikia Richard akihubiri kuhusu mada ya kubariki – kidogo mada isiyoumiza, lakini moja ambayo ilivuma kwa sababu ya namna ilivyokuja. Matokeo yalikuwa kwamba baraka haihitaji iwe kitu cha kumwuliza Mungu, lakini sisi kama Wakristo tuna mamlaka, kama si wajibu, kupeleka nje katika hii dunia iliyopotoka na kama mabalozi wa Kristo tufanye athari kwa maisha ya watu wengine binafsi kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Tunaweza kwenda nje na kuwabariki katika maisha yao, na kuwaonyesha Kristo wakati huo.*
>
> *Hilo wazo ni zuri mmoja anapowafikiria wen-*

*gine, lakini wazo hili liligonga ukuta wa matofali kwangu nilipokuwa nijifikirie mimi mwenyewe. Singeweza kuondoa wazo kwamba sikufaa, kwamba nilikuwa nakuwa mchoyo, kwamba nilikuwa namchukulia Mungu kuwa kawaida. Mawazo yangu yalibadilika nilipoona kwamba, kama Wakristo, tu kiumbe kipya, tumezaliwa tena na kuumbwa kwa kusudio ambalo Mungu ametupangia. Likiwa hivyo, mwili tulionao sasa ni ule tunatakiwa tuuthamini sana na tuutunze – sisi sasa, hata hivyo, hekalu la kukaa Roho Mtakatifu.*

*Baada ya hilo, nilianza jaribio fupi kila siku ningeamka, ningeibariki sehemu ya mwili wangu, niishukuru kwa utendaji wake; niisifu kwa kazi nzuri kufanywa. Ningesifu vidole vyangu kwa ubingwa, ufundi vilivyonavyo katika kufanya kila kazi vitakiwavyo kufanya na zaidi. Ningesifu miguu yangu kuwa ya kutochoka ya uchukuzi na mbio, kwa uwezo wayo kufanya kazi kwa pamoja. Niliusifu mwili wangu kwa sehemu zote kufanya kazi nzuri pamoja. Kitu kimoja cha ajabu kilitokea katika hili (jambo).*

*Kwa sababu nilijihisi bora zaidi kimaumbile na kiakili, niligeuza mawazo yangu kwa ule uchungu ambao nilikuwa nimekuwa nao kwa miezi kadhaa katika sehemu ya chini ya mkono wangu – uchungu ambao ni kama ulikuwa katika mfupa na ambao ulihitaji usuguliwe mara kwa mara angaa kwa kiasi kupunguza mpigo wa siku zote. Nililenga sehemu hii nikiusifu mwili wangu kwa uwezo wake wa kuponyesha, kwa ushupavu wake kushinda hivyo vitu vinavyotupwa dhidi yake kwa msaada ambao sehemu zingine zingetoa huku marekebisho yakifanyiwa sehemu nyingine. Ilikuwa karibu wiki tatu tu baadaye kwamba niliamka asubuhi moja kwa kugundua kwamba sikuwa tena nahisi uchungu katika mkono wangu; kwamba kuuma kulikuwa kumetoweka kabisa na hakujarudi.*

*Nilikuja kutambua kwamba ingawa kwa hakika upo muda na wakati kwa kipawa cha upon- yaji kuweza kutumiwa kupitia imani kwa ajili ya faida ya wengine, kuna pia njia nyingine wazi kwetu sisi kama watu binafsi kushirikisha kipawa cha uponyaji ndani yetu wenyewe. Ni funzo*

*katika unyenyekevu, kwamba tunaweza kuamini kile Mungu ameipa miili yetu mipya, kwamba tunaweza kwenda mbele katika matu- maini katika mtindo mpya na wenye uhai wa kuishi.*

**Kubariki nyumbani, ndoa na watoto wako**

***Nyumba yako – mfano hasa wa kubariki nyumba***
Ni wazo zuri kubariki nyumba yako na kukufanya upya kubariki huko angaa mara moja kwa mwaka. Kubariki pale mahali unapoishi kwa kawaida huhusisha utumiaji wa mamlaka yako ya kiroho katika Kristo Yesu kuweka wakfu na kufanya patakatifu mahali pale kwa Bwana. Ni kukaribisha Roho Mtakatifu kuja, na kulazimisha kila kitu kinginecho ambacho si cha Mungu kuondoka.

Nyumbani si matofali na mota tu – pia ina nafsi ya mtu. Kama tu ulivyo na njia ya kisheria ya kuifikia nyumba yako sasa, mtu mwingine alikuwa na njia ya kisheria ya kuifikia, au mali kabla ya wewe. Vitu vinaweza kuwa vilifanyika mahali humo ambavyo vilileta aidha baraka au laana. Bila kujali kilichofanyika,

ni mamlaka yako ambayo yanaamua mazingira ya kiroho yatakuwa vipi kuanzia sasa na kuendelea. Ikiwa kuna shughuli ya kishetani bado inaendelea tangu umiliki uliopita, utaweza kwa kiasi kikubwa labda kuihisi – na ni juu yako kuzifukuza nguvu hizi.

Bila shaka, utahitaji kufikiria ni nguvu gani za kishetani ambazo unaweza kuwa bila kujua wewe mwenyewe unazipa njia kuingia nyumbani kwako. Una michoro, vyombo, vitabu, nyimbo au video mbovu zisizofaa? Ni vipindi gani vya runinga uviruhusuvyo ndani? Iko dhambi nyumbani kwako?

Hapa pana baraka rahisi unayoweza kufanya una-potembea ndani ya nyumba yako chumba kwa chumba:

> *Naibariki nyumba hii, makao yetu. Ninatamka nyumba hii ni ya Mungu. Naiweka wakfu kwa Mungu na kuiweka chini ya Ubwana wa Yesu Kristo. Ni nyumba ya baraka.*
>
> *Ninavunja kila laana katika nyumba hii kwa damu ya Yesu. Ninachukua mamlaka juu ya*

*shetani yeyote na kila shetani katika jina la Yesu na kuyaamuru yaondoke sasa na yasirudi tena. Ninatupa nje kila roho ya mabishano, migawanyo na kutoelewana. Ninatupa nje roho ya umaskini.*

*Njoo Roho Mtakatifu na ufukuze kila kitu kisichokuwa cha kutokana na Wewe. Jaza hii nyumba na uwepo wako. Wacha tunda lako lije, upendo, furaha, amani, huruma, subira, wema, unyenyekevu, uaminifu na kujizuia. Naibariki nyumba hii na amani inayofurika na upendo uliojaa tele. Wote wanaokuja hapa wahisi uwepo wako na wabarikiwe. Katika jina la Yesu, amina.*

Nimetembea kuzunguka mpaka wa miliki yangu, nikiibariki na kiroho nikiweka damu ya Yesu Kristo kwa ulinzi wa miliki hiyo, na watu waliomo, dhidi ya kila ovu na dhidi ya misiba ya asilia.

***Ndoa yako***

*Tuna aina ya ndoa tunayoibariki au tuna aina ya ndoa tunayoilaani.*

Niliposoma habari hii kwanza katika *The Power of Blessing* (Nguvu ya Kubariki) na Kerry Kirkwood, nilishituka kidogo. Hii ni kweli?

Nimeifikiria sana, na ninaamini kwamba maneno haya ni ya kweli pakubwa huzuni yoyote katika ndoa yetu au watoto wetu ni kutokana na sisi kutozibariki na kutowabariki! Kwa kubariki, tunapokea uzuri kamili Aliotukusudia Mungu – Pamoja na maisha marefu na mahusiano mazuri. Tunakuwa washirika, au wenzi, wa tunavyovibariki na tunaowabariki.

Jihadhari na laana. Waume na wake wanajuana vizuri kabisa. Tunajua udhaifu wote. Wewe husema chochote kama hiki? Hivi ni aina ya vitu ambavyo huwahi kusemwa kwako? 'Kamwe husikilizi', 'Kukumbuka kwako ni ovyo', 'Huwezi kupika', 'Wewe ni bure katika…' Yakisemwa mara nyingi vya kutosha, maneno ya aina hizi huwa laana na huwa kweli.

Usilaani, bariki. Kumbuka, ukilaani (ukinena maneno ya mauti) hutarithi baraka ambayo Mungu anakutakia. Baya zaidi ya hilo, kulaani hutuathiri zaidi ya

yule tunaweza kuwa tunamlaani. Hiyo yaweza kuwa sababu ya maombi kuwa hayajibiwi?

Kujifunza kubariki kunaweza kuwa kama kujifunza lugha mpya – ngumu kuelewa mwanzoni. Kwa mfano:

> *Nicole ninakubariki. Ninaachilia wema wote wa Mungu juu yako. Mipango ya Mungu kwa maisha yako ipate kutoa mazao. Kipawa chako cha kukutana na kuwapenda watu. Ninabariki kipawa chako cha ukarimu. Ninabariki kipawa chako cha kuwafanya watu wajihisi katika utulivu. Ninataka wewe kama mhudumu wa kike wa Mungu, kwamba uwapokee watu jinsi Yeye Angewapokea. Ninakubariki na nguvu uweze kuendelea kufanya hivi hata katika miaka ijayo. Ninakubariki na afya na maisha marefu. Ninakubariki kwa mafuta ya furaha.*

***Watoto wako***

Zipo njia nyingi za kubariki mtoto. Hivi ndivyo nimbarikivyo mjukuu wangu wa kike, ambaye ana umri wa miaka minne:

*Ashley, ninabariki maisha yako. Ukaweze kuwa mwanamke wa ajabu wa Mungu. Ninabariki mawazo yako yabaki timamu na wewe uwe na busara na ufahamu katika maamuzi yote. Ninabariki mwili wako ubaki safi hadi ndoa na uwe na afya na nguvu. Ninabariki mdomo wako. Uweze kusema maneno ya ukweli na kutia moyo. Ninabariki moyo wako uwe kweli kwa Bwana. Ninambariki atakayekuwa mume wako na maisha ya usoni ya watoto wako na uta- jiri wa umoja. Ninapenda kila kitu kuku-husu, Ashley, na ninajivunia kuwa babu yako.*

Bila shaka, mahali mtoto anang'ang'ana katika shughuli fulani tunaweza kuwabariki ifaavyo. Iwapo wanapata shida katika masomo shuleni, tunaweza kubariki akili zao kukumbuka masomo na kuelewa mawazo yanayohusika katika mafunzo; iwapo wanadhulumiwa, tunaweza kuwabariki wakue katika busara na kimo na fadhila za Mungu na watoto wengine; na kadhalika.

Nakumbuka nikiongea na mwanamke wa ajabu wa Mungu kuhusu mjuku wake wa kiume. Yote ali-

yoyasema kumhusu mjukuu wake yalielekezwa kwa makosa, mwelekeo wake hasi, na tatizo yake ya tabia aliyokuwa nayo shuleni. Alikuwa ametumwa kwa kongamano ili aweze kurekebika na kunyooka, na akawa ametumwa nyumbani tena kwa sababu alikuwa mharibifu.

Baada ya kumsikiliza kwa mda fulani, nilipendekeza kwa mwanamke huyu kwamba alikuwa akimlaani pasipo kujua mjkuu wake kwa njia aliyokuwa akizungumza kumhusu, na alikuwa akimfunga kwa maneno yake. Hivyo, alikoma kunena kinyume, na badala yake alimbariki makusudi. Mume wake, babu wa mvulana huyu, akafanya sawa. Ndani ya siku chache , mvulana huyu alikuwa amebadilika kikamilifu, akirejea kwa kongamano na kunawiri. Zungumza kuhusu majibu ya haraka ya mastaajabu ya nguvu za kubariki!

Mojawapo ya vitu vizuri sana ambavyo baba anaweza kuwapa watoto wake ni baraka ya baba. Nimejifunza kuhusu hii kutoka *The Father's Blessing* (Baraka ya Baba) na Frank Hammond, ambacho ni kitabu kizuri sana. Bila baraka ya baba huwa kuna kuhisi kukosekana kwa kitu fulani; uwazi unaumbwa ambao hakipo kitu

kingine kinachoweza kuujaza. Akina baba, wawekeeni mikono watoto wenu, na watu wa jamaa (k.m. weka mkono wako katika vichwa au mabega yao) na uwabariki mara kwa mara. Gundua vitu vizuri ambavyo Mungu atafanya kwenu nyote wewe na wao.

Kila nisimuliapo ujumbe huu, huwa nawauliza wanaume na wanawake wazima, 'Ni watu wangapi hapa wamewahi kupata baba zao wakiwawekea mikono na kuwabariki?' Watu wachache sana huinua mikono yao. Kisha ninabadilisha swali, 'Ni watu wangapi hapa hawajawahi kupata baba zao wakiwawekea mikono na kuwabariki?' Karibu kila mtu huinua mkono wake.

Halafu ninauliza iwapo wangekubali niwe baba wa kiroho kwao katika wakati huo – mbadala – ndipo niweze katika nguvu za Roho Mtakatifu, kuwabariki na baraka ambayo hawajawahi kuwa nayo. Hilo limekuwa la kushinda kabisa: machozi, ukombozi, furaha, uponyaji. Kustaajabisha tu!

Iwapo unatamani sana baraka ya baba, jinsi nilivyotamani sana, basi sema yafuatayo kwa sauti juu

yako wewe mwenyewe. Ni baraka ambayo nime-badili kutoka katika kitabu cha Frank Hammond.

**Baraka ya baba**

*Mtoto wangu, ninakupenda! Wewe ni wa kipekee. Wewe ni zawadi kutoka kwa Mungu. Ninashukuru Mungu kwa kunikubali kuwa baba kwako. Ninakujivunia na kufurahia juu yako. Na sasa ninakubariki.*

*Ninakubariki na uponyaji wa vidonda vyote vya moyo – vidonda vya kukataliwa kutelekezwa na kutukanwa ambayo umeumia, katika jina la Yesu, ninavunja nguvu zote za maneno ya dhuluma na uonevu usiostahili yaliyonenwa juu yako.*

*Ninakubariki na amani inayofurika, amani ambayo Mfalme wa Amani pekee anaweza kupatia. Ninabariki maisha yako na uzao wa matunda, matunda, mazuri, matunda kwa wingi na matunda ya kudumu.*

*Nakubariki na mafanikio. Wewe ni kichwa na si mkia; Uko juu na si chini. Ninabariki vipawa ambavyo Mungu amekupa. Ninakubariki na busara kutoa maamuzi mazuri na kuendeleza uwezo wako kikamilifu katika Kristo.*

*Ninakubariki na ufanisi unaofurika, una- okuwez- esha kuwa baraka kwa wengine. Ninakubariki na ushawishi wa kiroho, kwa kuwa wewe ni nuru ya dunia na chumvi ya ulim- wengu. Ninakubariki na ufahamu wa kiroho wa kina na matem- bezi ya karibu na Bwana wako. Hutajikwaa au kusita, ambavyo Neno la Mungu litakuwa taa kwa nyayo zako na nuru kwa njia ya miguu. Nakubariki na marafiki wazuri. Una fadhila ya Mungu na ya mwanadamu.*

*Ninakubariki na upendo tele na unaofurika, kutokana nao utahudumu neema ya Mungu kwa wengine. Utahudumu neema ya Mungu inayofariji kwa wengine. Umebarikiwa, mwa- nangu, Umebarikiwa na baraka zote za kiroho katika Kristo Yesu. Amina!*

***Ushuhuda kuhusa thamani ya baraka ya baba***

*Nilibadilishwa na baraka ya baba. Tangu nizaliwe nilikuwa sijawahi kusikia ujumbe kama huu ukihubiriwa. Sijawahi kuwa na baba mzazi atamke katika maisha yangu kufika hapa nilipo sasa. Mungu alikutumia wewe, Richard, kunileta hadi kufikia kiwango ambapo nilihitaji baraka ya baba juu ya maisha yangu. Ulipoachilia baraka ya baba-kwa-mwana, moyo wangu ulifarijika na sasa nina furaha na nimebarikiwa. – Pasta Wycliffe Alumasa, Kenya*

*Ulikuwa mwendo mrefu na mgumu kung'ang'ana na huzuni; vita iliyopiganwa kwa upande mwingi- mawazo, roho, mwili. Kuponywa hali yangu ya kale kulikuwa muhimu na nilipiga hatua muhimu mbele kuliko tu kule kumsamehe baba yangu-sio tu kwa maovu aliyokuwa amefanya hapo awali, bali kwa mambo ambayo hakuwa amefanya. Babangu hakuwahi niambia kuwa ananipenda. Hisia zake zilikuwa zimefungika. Hata hangeweza kupata maneno ya upendo, ya kunijali na kunili-*

*waza ambayo angeniambia-ingawa nilitamani moyoni mwangu kuyasikia.*

*Lakini kupitia kwa msamaha na moyo wangu kupona, huzuni iliniondokea ijapokuwa nilikuwa ningali nazo dalili za ugonjwa wa 'irritable bowel syndrome' katika mwili wangu. Daktari alikuwa ameniandikia dawa na lishe maalum ambayo ilinisaidia tu padogo, nikawa nimeambiwa kuwa ingesaidia kupambana na dalili za ugonjwa ila si kuuponya.*

*Rafiki yangu Richard alikuwa ameniambia kwa muda habari za baraka za baba, na jinsi watu walivyokuwa wameitikia kutokana na matokeo yake. Moyoni mwangu nilishikilia wazo hilo. Lakini nilifahamu fika kuwa, nikiwa nimemsamehe baba yangu kwa pengo alilokuwa ameliacha, hakika sikuwa nimeliziba pengo hilo wala kuridhisha tama ya moyo wangu. Na ikatokea siku moja asubuhi katika mkahawa wakati wa kiamsha kinywa, Richard alisimama katika nafasi ya babangu ambayo hangeweza kujaza na kunibariki kama mwanawe. Roho*

*wa Bwana alinishukia na kukaa nami mchana kutwa. Ilikuwa hali nzuri sana niliyoipitia na ile sehemu katika moyo wangu iliyokuwa ikiomboleza ikatulia na kuwa na amani.*

*Matokeo yasiyotarajiwa yakatokea kwamba hata dalili za ugonjwa ulionileta mwasho ndani ya utupu wangu ukaisha kabisa. Yale matibabu niliyokuwa nikiyapata pamoja na mapendekezo ya daktari ya lishe yakatoweka. Moyo wangu ulipopata ulichokihitaji, mwili pia ukapona. – Ryan*

**Kubariki wengine kwa kuachilia kinabii**

Ingawa nimetoa mifano kukusaidia upate kuanza, ni vyema kumwuliza Roho Mtakatifu kukusaidia kuwa kama mdomo wa Mungu, kutamka na kuachilia kusudio maalumu la Mungu au 'neno katika msimu' (neno jema katika wakati sahihi). Ikiwa hali inaruhusu, chochea roho yako kwa maombi katika ndimi au ibaada.

Unaweza kuanza kwa kutumia mifano mbalimbali ya awali, lakini amini kwamba Roho Mtakatifu atakuele-

keza. Sikiza mpigo wa moyo Wake. Unaweza kuanza kwa kusitasita, lakini utashika hivi karibuni moyo wa Bwana.

**Kubariki mahali pako pa kazi**

Rejelea Sehemu ya kwanza na utumie mfano niliotoa, kutoka katika tukio langu mwenyewe, katika hali zako. Uwe wazi kwa yale Mungu Akuonyeshayo – Anawaza kubadilisha taswira yako. Kubariki si aina fulani ya laana ya kichawi. Kwa mfano, Mungu hatafanya watu wanunue wasichohitaji au wasichotaka. Wala Mungu hatabariki uvivu na udanganyifu. Lakini ukitimiza mahitaji Yake basi [wewe] ubariki biashara yako. Kwamba Mungu Atakusaidia. Akiitoa mahali ilipo sasa hadi Anapotaka iwe. Sikiliza upate ushauri. Wake au ushauri wa watu anaowatuma kwako. Uwe wazi. Lakini tena tarajia fadhila Yake, kwa sababu Anakupenda na Anataka ufaulu.

Nilipata ushuhuda ufuatao kutoka kwa Ben Fox:

> *Kazi yangu halisi katika tasnia ya mali ilipata mabadilko katika miaka michache iliyopita*

*na kulikuweko na kiasi kikubwa cha kushuka katika biashara yangu. Nilikuwa nimeenda kwa watu kadhaa waombee kazi yangu kwa sababu shughuli zilikuwa zinapunguka kufikia kiasi cha kunisumbua na kunitia wasiwasi. Karibu wakati huo, mapema 2015, nilisikia Bwana Brunton akihubiri mfululizo wa jumbe kuhusu kubariki kazi, biashara, jamaa na sehemu zingine za mtu. Hadi wakati huo, lengo la maombi yangu lilikuwa kuuliza Mungu ani- saidie katika sehemu hizi. Wazo la sisi wenyewe kutamka baraka halikuwa limefunzwa kwangu, lakini naweza sasa kuona limeandikwa kotekote katika Biblia, na ninajua kwamba Mungu hutu- ita sisi, na Ametupa mamlaka, kufanya hivyo katika jina ya Yesu. Kwa hivyo nilianza kubariki kazi yangu – kunena neno la Mungu juu yake na kushukuru Mungu kwayo. Niliendelea na kubariki kazi yangu kila asubuhi na pia kushuk- uru Mungu kwa biashara mpya, na kumuuliza anitumie wateja ambao ningewasaidia.*

*Katika miezi kumi na miwili iliyofuata, kiwango cha kazi kiliongezeka vya kuridhisha na tangu*

*wakati fulani nimepata kulemewa na kiasi cha kazi ambayo hunijia. Nimejifunza kwamba kuna njia ya kumshirikisha Mungu katika shughuli zetu za kila siku, na kubariki kazi yetu ni sehemu ya yale Mungu hutuita kufanya. Kwa hivyo ninampa Mungu sifa zote nzuri. Pia nilianza kumwalika Roho Mtakatifu katika siku yangu ya kazi, nikiomba busara na mawazo mabunifu. Hasa, nimefahamu kwamba nikiomba Roho Mtakatifu kunisaidia na utendaji bora wa kazi yangu, kwa kawaida mimi huikamilisha vizuri kabla ya muda uliotarajiwa.*

*Inaonekana kwangu kwamba ufundishaji wa kubariki, na jinsi ya kubariki umesahauliwa na makanisa mengi kwa kuwa Wakristo wengine niwambiao hawana habari. Kubariki kazi yangu kumekuwa sasa tabia yangu ya kila siku, sawa na kubariki wengine. Ninatazamia kwa tarajio kuona tunda katika watu na vitu vinavyobariki vinapokuwa kulingana na Neno la Mungu katika jina la Yesu.*

**Kubariki jumuia**

Hapa ninafikiria kuhusu kanisa – au chama cha aina hiyo – kubariki jumuia ambamo inafanya kazi.

*…… watu wa (jumuia), tunawabariki katika jina la Yesu kujua Mungu, kujua makusudio yake kwa maisha yenu, na kujua baraka zake juu ya kila mmoja wenu, jamaa zenu na hali zote za maisha yenu.*

*Tunabariki kila nyumba wanamoishi watu wa jamaa moja …… (jamii). Tunabariki kila ndoa na kubariki mahusiano katika watu wa jamaa wa vizazi tofauti.*

*Tunabariki afya yenu na mali zenu.*

*Tunabariki kazi za mikono yenu. Tunabariki kila shughuli yote iletayo afya mnayohusika nayo. Zikaweze kustawi.*

*Tunabariki wanafunzi katika shule zenu; tunawabariki wajifunze na waelewe yale ambayo wanasomeshwa. Wakue katika hekima na kimo*

*na katika fadhila ya Mungu na mwanadamu. Tunawabariki waalimu na kuomba kwamba shule ziwe mahali salama na penye afya, ambapo imani katika Mungu na katika Yesu inaweza kufundishwa kwa raha. Tunanena kwa mioyo ya watu walio katika jamii. Tunawabariki wawe wazi kwa kubembel- eza kwa Roho Mtakatifu na kuwa zaidi na zaidi wa kuitikia sauti ya Mungu. Tunawabariki na kufurika kwa Ufalme wa Mbinguni tunaou- uona hapa …… (kanisa).*

Bila shaka kubariki kwa aina hii, kufanywe desturi ya aina fulani maalumu ya jamii. Kama ni jamii ya wakulima, unaweza kubariki ardhi na mifugo; kama ni katika jamii kuliko na ukosefu mkubwa wa kazi basi bariki biashara ziunde kazi (za uajiri). Lenga kubariki kwa hitaji. Usijali kama wanastahili au la! Watu watahisi mioyoni mwao mahali ambako baraka imetoka.

**Kubariki ardhi**

Katika Mwanzo, tunaona Mungu akibariki wanadamu; akiwapa mamlaka juu ya ardhi na vitu vyote viishivyo, na kuwaamuru kuwa wa kuzaa matunda

na kuongezeka. Hii ilikuwa hali mojawapo ya sifa kuu halisi ya wanadamu.

Nilipokuwa Kenya hivi karibuni, nilikutana na mmishenari aliyewachukua machokora na kuwafundisha kuhusu kilimo. Alinisimulia hadithi ya jamii ya Kiislamu ambayo ilidai ardhi yao ilikuwa imelaaniwa, kwa sababu chochote hakikuweza kukua hapo. Rafiki yangu mmishenari na jamii yake ya Kikristo walibariki ardhi hiyo na ilikuja kuwa yenye rutuba. Hili lilikuwa onyesho la kuvutia liloonyesha kuachiliwa kwa nguvu za Mungu kwa kubariki.

Nikiwa Kenya, pia nilitembea kote katika makao ya mayatima ambayo kanisa letu linafadhili, nikibariki shamba lao la miti ya matunda, shamba lao, kuku na ng'ombe wao. (Nimebariki miti yangu mwenyewe kwa matokeo mazuri sana.)

Geoff Wiklund husimulia kisa cha kanisa moja huko Ufilipino ambalo lilibariki kipande cha ardhi ya kanisa wakati wa kiangazi kikubwa. Ardhi yao pekee ndiyo iliyopata mvua. Wakulima jirani walikuja kuchota maji kwa ajili ya mpunga wao kutoka mitaro iliyozunguka

ukuta wa ardhi ya kanisa. Huu ni muujiza mwingine mkubwa ambamo fadhila ya Mungu iliachiliwa kupitia kubariki.

**Kubariki Bwana**

Ingawa nimeacha hii mpaka mwisho, ilifaa hasa ije kwanza. Sababu ya kuiweka mwisho, hata hivyo, ni kwa kuwa hakuonekani kulingana na mfano wa 'kunena makusudio au fadhila ya Mungu kwa mtu au kitu'. Kidogo ni wazo la 'kufurahisha'.

Tunambarikije Mungu? Njia moja ya kufanya hivi imeonyeshwa katika Zaburi 103:1-2:

> *Ee nafsi yangu, mbariki Bwana; wala usizisahau fadhili zake zote…*

Fadhili za Mungu kuelekea roho zetu ni nini? Yeye husamehe, huponya, huokoa, hutawaza, hutosheleza, hufanya upya.

Mimi huhakikisha ninafanya zoezi la kukumbuka na kushukuru Mungu kila siku kwa yale ayafanyayo

ndani yangu na kupitia kwangu. Ninakumbuka na kufurahia kwa vyote ambavyo Yeye Yu kwangu. Hili humbariki, na mimi pia! Unahisije mtoto anaposhukuru au kukufurahia kwa kitu ambacho umefanya au umesema? Huchangamsha moyo wako na kufanya utake kumfanyia zaidi.

**Neno la mwisho kutoka kwa msomaji**

*N ivigumu kueleza jinsi baraka zilivyobadilisha maisha yangu. Katika maisha yangu, hakuna aliyekataa kubarikiwa kila nilipojitoa kubariki-Hata wakati mmoja nilipata nafasi ya kumbariki mwanamume wa kiislamu. Kujitolea katika maombi ya kubariki maisha ya mtu hufungua milango… ni kitu na njia rahisi isiyotisha katika kuleta Ufalme wa Mungu maishani mwa mtu. Kwangu, kuwezeshwa kuombea watu baraka kumeniongezea ala maalumu katika kisanduku changu cha zana za kiroho….ni kana kwamba hapo awali kulikuwa na kitu fulani nilicho kikosa maishani na sasa kimeingizwa mahali pake… – Sandi*

# KUTUMIA

- Fikiri juu ya mtu ambaye amekuumiza – samehe ikilazimu, lakini enda zaidi na uwabariki.

- Pima vitu usemavyo mara kwa mara ambapo huwalaani wengine au hujilaani mwenyewe. Utafanya nini kuyahusu?

- Andika baraka kwako wewe, kwa mume au mke wako, na kwa watoto wako.

- Kutana na mtu mwingine na uwe wazi kwake. Muulize Mungu ufunuo wa kitu maalumu na cha kutia moyo kwa mtu huyo. Anza kwa kuongea kwa jumla, kwa mfano, 'Ninakubariki katika jina la Yesu. Mipango ya Mungu na makusudio Yake kwa maisha yako ya kuzaa matunda…' na subiri, uwe na uvumilivu. Kumbuka una akili ya Kristo. Halafu badilisha nafasi, na upate huyo mtu mwingine akubariki kinabii.

- Katika kanisa lako, una shirika la kubariki maeneo na kuponya jimbo lako au bariki wito ambao tayari uko nao.

# NAMNA YA KUWA MKRISTO

Hiki kitabu kidogo kiliandikiwa Wakristo kuwa 'Wakristo'; sina maana tu watu wanaoishi maisha mazuri. Ninamaanisha watu ambao 'wamezaliwa tena' kwa Roho wa Mungu na wanapenda na kumfuata Yesu Kristo.

Watu wameumbwa katika sehemu tatu: roho, nafsi na mwili. Sehemu roho ilikusudiwa kujua na kujisikia kuwa pamoja na Mungu Mtakatifu ambaye ni Roho. Wanadamu waliumbwa kwa ajili ya kuwa na urafiki wa karibu sana na Mungu, roho kwa Roho. Hata hivyo, dhambi ya kibinadamu hututenganisha na Mungu, matokeo yakiwa ni mauti ya roho na kupoteza urafiki na Mungu.

Kwa hivyo, watu huelekea kufanya mambo yao kutokana na nafsi zao na miili yao pekee. Nafsi huwa na akili, nia na hisia. Matokeo ya hili ni wazi kabisa katika

ulimwengu: uchoyo, majivuno, ulafi, njaa, vita na ukosefu wa amani ya kweli na maana.

Lakini Mungu ana mpango kuwakomboa wanadamu. Mungu Baba alimtuma mwanawe, Yesu, ambaye pia ni Mungu, kuja duniani kama mtu kuonyesha jinsi Mungu Alivyokuwa – *'kama umeniona Mimi umemwona Baba'* – na kuchukua juu Yake matokeo ya dhambi yetu. Kifo chake kibaya msalabani kilipangwa tangu mwanzoni kabisa na kilitabiriwa katika Agano la Kale. Alilipa gharama ya dhambi ya wanadamu. Haki ya Mungu ilitosholezwa.

Lakini wakati huo Mungu Alimfufua Yesu kutoka wafu. Yesu Anaahidi kwamba wale wanaoamini katika Yeye pia watafufuliwa kutoka wafu kuishi milele nayeye. Hutupa Roho Yake sasa, kama dha- mana, ili kwamba tuweze kumjua na kutembea naye kwa sehemu iliyobaki ya maisha yetu duniani.

Kwa hivyo, hapo tuna kiini cha Injili ya Yesu Kristo. Iwapo utakiri na kutubu dhambi yako, ukiamini kwamba Yesu alikuchukulia adhabu yako katika msalaba na kwamba Alifufuliwa kutoka wafu,

hivyo ukamilifu Wake utadhaniwa kwako. Mungu Atamtuma Roho Mtakatifu Wake kufufua roho yako ya mwanadamu – hiyo ndiyo maana ya kuzaliwa tena na utaweza kuanza kujua na kijisikia kuwa karibu na Mungu kirafiki – ambayo ndivyo sababu kwanza kabisa alikuumba wewe! Mwili wako wa kimaumbile unapokufa, Kristo Atakufufua na kukupa ule ulio mtakatifu, usioharibika. Lo!

Unapoendelea kuwa katika hii dunia, Roho Mtakatifu (ambaye pia ni Mungu) Atafanya kazi ndani yako (kukusafisha na kukufanya zaidi kama Yesu katika tabia) kupitia kwako (kuwa baraka kwa wengine).

Wale ambao wanaamua kutopokea kile alicholipia Yesu wataenda hukumuni pamoja na matokeo yake. Hulitaki hilo.

Hapa pana dua unayoweza kuomba. Iwapo utaomba kwa ukweli utazaliwa tena.

> *Mpendwa Mungu uliye mbinguni, naja kwako katika jila la Yesu. Ninakiri kwako mimi ni mwenye dhambi. (Tubu dhambi zako zote ziju-*

*likanazo). Ninasikitika kikweli kwa dhambi zangu na maisha ambayo nimeishi bila wewe na ninahitaji msamaha wako.*

*Ninaamini kwamba Mwanao Wa pekee, Yesu Kristo, Alimwaga damu Yake ya thamani kubwa katika msalaba na Alikufa kwa dhambi zangu na sasa ninahiari kuacha dhambi yangu.*

*Ulisema katika Biblia (Warumi 10:9) kwamba tukitamka kwamba Yesu ni Bwana na kuamini katika mioyo yetu kwamba Mungu Alimfufua Yesu kutoka katika wafu, tutaokolewa.*

*Hivi sasa ninamkubali Yesu kama Bwana wa nafsi yangu. Ninaamini kwamba Mungu Alimfufua Yesu kutoka katika wafu. Sasa hivi ninampokea Yesu Awe Mwokozi wangu bin-afsi, na kulingana na Neno Lake, mara hii nimeokoka. Asante Bwana, kwa kunipenda sana kiasi kwamba ulihiari kufa kwa niaba yangu. Unastaajabisha, Yesu, na ninakupenda.*

*Sasa ninakuomba unisaidie kwa Roho Yako*

*niwe mtu ambaye Ulikusudia mimi kuwa tangu kabla mwanzo wa wakati. Niongoze hadi kwa waumini wenzi na kanisa la chaguo Lako kwamba nikue ndani Yako. Katika jina la Yesu, amina.*

Asante kwa kukisoma hiki kitabu kidogo.
Ningependa nipate shuhuda kuhusu jinsi
kubariki kulivyobadilisha maisha yako,
au maisha ya wale umewabariki.
Tafadhali wasiliana nami kupitia:

richard.brunton134@gmail.com

## Kubariki ni kunena makusudio au fadhila ya Mungu kwa mtu au hali fulani.

Tunapofanya hivyo katika imani, tunachochea nguvu za Mungu kubadilisha mtu (pamoja na sisi) tukiwemo au hali, kutoka alipo sasa hadi anapotaka Mungu awe.

Kila Mkristo ana mamlaka na nguvu ya kuwabariki wengine katika jina la Bwana na kuona maisha na hali ikibadilika. Nguvu za baraka ni za mwujiza; ni uwepo na kazi ya Roho Mtakatifu, zikitoa furaha, amani, ufanisi na matokeo mazuri na kutoa afya, mafanikio na ulinzi.

Katika hiki kitabu kidogo, utapata kugundua jinsi kubariki kufanyavyo kazi na kujifunza jinsi ya kuwabariki wale ambao hukulaani au kukutusi, jinsi ya kumbariki mume au mke, watoto wako, makao yako na wewe mwenyewe, jinsi ya kubariki mahali pako pa kazi, shamba lako na jumuia yako – na hata Mungu Mwenyewe.

**Unaweza kuibadilisha dunia yako.**

ISBN 978-0-473-42987-4

9 780473 429874 >

SWAHILI VERSION
SECOND EDITION